plan:g
Partnership
for Global Health

Picha/Taswira na Ujumbe

Mkataba wa Mwongozo

1. Dibaji

Huu ni mkataba wa mwongozo kuhusu picha/taswira na ujumbe ulioanzishwa na shirika lisilo la kiserikali la ki-Irish DOCHAS (Irish NGO DOCHAS). Baadhi ya mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yamekuwa yakifanya kazi kwa kutoa misaada kwenye maeneo ya dharura: maendeleo ya muda mrefu na maendeleao ya kielimu. Mashirika haya yamechangia kwenye maendeleo ya mkataba huu. CONCORD ilihidhinisha muungano wa mashirika yasiyo ya kiserikali. DOCHAS iliendeleza mwongozo kwa kutekeleza mkataba huu http:/dochas.ie/Shared/Files/5/Guide To Code.pdf

Lengo la mkataba wa mwongozo huu ni kutoa maelekezo ambayo mashirika yanaweza kufuata wakati wa ubunifu na utekelezaji wa mkakati wa mawasiliano yao kwa umma. Mkataba unatoa mwelekezo wa mwongozo ambao unaweza kusaidia wafanyakazi katika jitihada zao za kuwasiliana na utaratibu wa mashirika yao kwa manufaa na pia katika kuambatana na njia iliyo bora.

Waweka sahihi kwenye mkataba huu wanatambua wingi wa changamoto na ugumu unaofanyika katika ubebaji wa kashfa na udhalimu wa umaskini wakati huo huo wakipambana kufikia malengo ya mkataba huu. Ni hali halisi katika ulimwengu wetu wa sasa ya kwamba picha/taswira nyingi za umaskini wa kupindukia, na picha/taswira za maafa ni za kuhuzunisha mno haziwezi kupuuziwa. Kwa kuzipuuzia itapelekea kupinga lengo hili la mkataba huu ambalo unapaswa kuonyesha ukweli wa maisha ya watu kwa kuguswa na kuheshimu hadhi ya utu wao.

Picha/taswira na ujumbe vinapaswa kuwakilisha picha kamili ya pande zote mbili za usaidizi wa ndani na nje, na uhusiano ambao utakuwa wa kufanyakazi pamoja na mashirika ya siyo ya kiserikali ya ndani ya nchi na ya nje ya nchi.

Thamani ya hadhi ya utu wa binadamu, heshima na ukweli kama ulivyo muhtasari katika mkataba huu, lazima usisitizwe kwenye mawasiliano yote. Watia sahihi kwenye mkataba huu wanaahidi kwenye hizi kanuni , na watazitafsiri katika sera na taratibu za ndani. Na pia wanatoa ahadi ya kufanya kazi na wengine kwa kutoa maoni yatakayosaidia wale ambao kazi zao zinahusisha mawasiliano kwenye masuala ya umasikini ulimwenguni, na kwa njia ya uchunguzi wa kutafakari kanuni hizi katika maeneo mengine ya mawasiliano.

Kwa kutia sahihi na kuendeleza mkataba huu, mashirika yasiyo ya kiserikali (NGOs) yataendeleza sana ajenda ya maendeleo kwa umma. Wataangalia kwa mtazamo wa mbali

zaidi kuliko kuzingatia sehemu ndogo ya taarifa kutokana na manufaa yaliyotajwa katika mkataba huu.

## 2. Mkataba wa Mwongozo katika Picha/taswira na Ujumbe

### a. Kanuni za Mwongozo

Uchaguzi wa picha/taswira na ujumbe utafanyika kwa misingi muhimu ya kanuni za:

- Heshima kwa hadhi ya utu kwa watu wanaohusika
- Imani katika usawa wa watu wote
- Kukubalika kwa mahitaji ya kuendeleza haki, umoja na utendaji haki

Kutokana na mawasiliano yetu yote ambayo yanatendeka kama inavyotakiwa kulingana na mahitaji yanayoikabili hali halisi, tunapambana na;

- Chagua picha/taswira na ujumbe unaohusika kwenye misingi ya usawa na heshima, umoja/mshikamano na utendaji haki.
- Ukweli huwakilisha picha yoyote au kwa hali ya ufafanuzi kwa pande zote mbili, kwa haraka na kwa kiasi kikubwa cha kuendeleza kuelimisha umma katika hali halisi na vipengele tofauti vya maendeleo.
- Epukana na picha/taswira na ujumbe ambao unaweza kugusia hali ya ubaguzi kati ya watu au hali mbaya ya kuaibisha.
- Tumia picha/taswira, ujumbe na utafiti wa mambo muhimu wenye kueleza vizuri hali halisi, pia washirikishe wahusika na pata ruhusa toka kwao. Kwa wale wahusika ambao wana umri mdogo, pata ruhusa kutoka kwa wazazi au walezi wao.
- Hakikisha wale ambao wamehusishwa wapewe fursa ya kusimulia habari zao wenyewe.
- Anza kuweka kumbukumbu kama mhusika angependa kutajwa au kuonyeshwa, kila mara fanya inavyopaswa kuwa.
- Fuata kiwango cha juu kinachohusu haki za watoto kutokana na Makubaliano ya Haki za Mtoto (CRC); kwani watoto ndio wahusika mara kwa mara.

### b. Tamko la Ahadi

Sisi kama waweka sahihi kwenye mkataba wa CONCORD, tunathibitisha kwa kutoa ahadi yetu ya kuwa na utendaji mzuri wa mawasiliano na ushirikiano wa shirika letu zima.

Kwa kuweka sahihi kwenye mkataba huu, tunaahidi kwamba tutafuata utekelezaji wa mfumo mzima unaofanya kazi kama inavyotakikana, na kwa kuhakikisha kwamba kanuni za mkataba huu zinatekelezwa katika shughuli zozote za shirika letu.

Wajibu wetu kama waweka sahihi katika mkataba huu, unatuongoza kwa kuwajibika kwenye mawasiliano yetu kwa umma kama ifuatavyo:

1. Tutafanya kuwepo kwa mkataba wa CONCORD kujulikane kwa umma kwa kuwaambia watu wote na kuwapatia njia ya kutoa maoni ambayo mtu yeyote anaweza kutoa maoni kama mkataba huu unafuatwa au la, na mwananchi yeyote atakuwa na "haki kutoa changamoto" kwa matumizi ya mkataba wetu.
2. Tunaahidi kwamba ni wajibu wetu kuwasiliana na wahusika wote kuhusu mawasiliano mazuri ya picha/taswira na ujumbe katika taarifa ya sera kwa umma, kwa kuweka taarifa zifuatazo za mawasiliano husika ya umma (taarifa za kila mwaka, tovuti, taarifa za sera, nyaraka za utawala, vipeperushi na nyenzo nyingine za mawasiliano):
   „Aussatzigen-Hilfswerk Osterreich imetia sahihi mkataba wa mwongozo kwenye picha/taswira na ujumbe. Tafadhali tuma maoni yako kwa www.plan-g.at/program-contact
3. Tunaahidi kukagua mawasiliano yetu kwa umma kila mwaka kutokana na kanuni za mwongozo.
4. Tutaweka kumbukumbu za ufuatiliji kwenye mkataba katika kanuni za mwongozo wa shirika letu na kuhakikisha kwamba uongozi wa juu unakuwa na jukumu la utekelezaji na ufuatiliaji wa mkataba.
5. Tutahakikisha kwamba wahusika wote kama wagawaji, makontrakta na vyombo vya habari wafuate mkataba huu wakati wanafanya kazi na shirika letu.
6. Tunaahidi kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wetu kwa matumizi ya picha/taswira na ujumbe.
7. Tunaahidi kukutana katika kila mwaka na kubadilishana mawazo ya uzoefu wetu kwa kutumia na kutekeleza mkataba huu pamoja na waweka sahihi wa mashirika mengine.